# UFALME WA MUNGU

UTANGULIZI;

Kabla ya chochote kuwepo kulikuwapo na Mungu, biblia inasema hapo mwanzo Mungu aliziumba mbingu na nchi, ukiingia ndani zaidi katika mtari huu utagundua kuwa kabla ya mwanzo wenyewe kulikuwapo na Mungu na yeye ndiye aliyeuumba mwanzo.

Biblia inamtambulisha Mungu kama alfa na omega yaani mwanzo na mwisho, yeye ndiye anayetengeneza mwanzo wa kitu na mwisho wake. Mungu huujua mwisho wa kitu kabla hajakiumba kitu chenyewe na chochote anachokiumba Mungu ni kwa hakika kuwa ameshakitengeneza hata mwisho wake. Mungu anapokuruhusu kufanya jambo fulani huna haja ya kuhofia na kuwa na mashaka kwasababu yeye amesha kimaliza na amekupa wewe ukianze.

Ndio maana hupaswi kuwa na mashaka na kuzaliwa kwako, kwa sababu kama Mungu ameruhusu hivyo basi ni hakika kuwa amekuandalia mwisho mwema, ni kazi yako kumwendea na kumsihi akupe vile alivyovipanga na kuviandaa kwa ajili yako.

Kama Mungu ndiye mwanzo au mwanzilishi wa vitu vyote basi tunavitu muhimu vya kujifunza. Kwanza Mungu alipomuumba mwanadamu alimpa akili yaani uwezo wa kufikiri, vitu vyote vya ajabu na kutisha ambavyo watu wanavifanya na kuvitengeneza ni matokeo ya akili ambayo mwanadamu alipewa na Mungu. Kama ndivyo basi tunahaja ya kumuogopa zaidi Mungu kwasababu akili ya mwanadamu ni kazi ya mikono yake, je uwezo wa Mungu ukoje? Biblia meeleza vizuri kuhusu uwezo wa Mungu, uwezo wake hauna kipimo.

Yeye ni Mungu na sisi tu wanadamu, kuna vitu amevifunua kwetu na kuvielezea kumuhusu ili tumfahamu na hivyo tuwe na ufahamu huo katika kila jambo tutakalolifanya kumuhusu.

Tukimfahamu Mungu na namna anavyotenda kazi tutajua kwanini alituumba na tunapaswa kufanya nini kwa ajili ya uumbaji wake. Kuna kusudi la Mungu kumuumba mwanadamu. Katika kitabu cha mwanzo 1:26 anasema na tumfanye mtu kwa mfano wetu na kwa sura yetu.... Ufunguo hapa ni kuwa ni ngumu mwanadamu kujifahamu yeye binafsi kama bado hajamfahamu aliye muumba kwasababu aliumbwa kwa mfano wake na kwa sura yake.

Ukitaka ujifahamu wewe vizuri ni muhimu ukamfahamu vizuri aliyekutengeneza, sisi tu wazao wa Mungu na tukitaka tuzijue tabia tunazotakiwa kuwa nazo ni muhimu tukamchunguza ili tuzifahamu tabia alizonazo aliye tuumba. Ukitaka kujifahamu wewe ni nani rudi ukamsome na kujifunza kumuhusu Mungu aliyekuumba kwasababu moja muhimu aliye kutengeneza au kukuumba wewe anakujua vizuri mno kuliko wewe unavyojijua, yeye ndiye anayejua maisha yako na hatima yako.

Hivyo kutokana na uhitaji huo wa kujifahamu nimeona ni muhimu tukajifunza kwa sehemu kuhusu Mungu ili wewe ujigundue ndani ya Mungu, ukipata ufahamu juu ya Mungu hutakuwa na makisio tena kuhusu Mungu, utajua hakika kitu sahihi cha kufanya kwa Mungu kwa ajili ya ubora wa maisha yako na mahusiano yako na Mungu.

Ambatana nami tujifunze pamoja kuhusu Mungu na ufalme wake katika kitabu hiki.

Emmanuel Minga.

UHITAJI WA ASILI.

Kuna kitu mwanadamu anakitafuta, kitu hiki ni asili ambayo anadhani aliwahi kuwa nayo hapo kwanza, ingawa hajui ni wapi na lini aliwahi kuwa na hicho kitu. Hivyo akainuka na kubuni mifumo ya kila aina ili tu kukitafuta kitu hicho ambacho anadhania kuwa aliwahi kuwa nacho, na anaamini kuwa akikipata atakuwa amepata hazina ya maisha.

Utafutaji huo ndio chanzo cha kuanzilishwa kwa dini mbalimbali ulimwenguni, hiyo yote ni kutafuta hicho kitu ambacho mwanadamu anakihisi alikipoteza huko mwanzoni kwa wakati usio julikana. Mwanadamu anahisi aliwahi kukimiliki kitu fulani ndani yake ambacho kilikuwa ni ufunguo wa maisha yake ulimwenguni.

Na kutokana na kukikosa hicho kitu mwanadamu anayachukia maisha kwa sababu kunakitu kakikosa ambacho kingemsaidia kudhibiti matatizo yaliyo mzunguka. Mwanadamu anachukia kuonewa, kugandamizwa, na vitu vingine vingi vinavyomkosesha uhuru wa kuishi maisha yake binafsi kwa furaha.

Kuna kitu cha thamani mno mwanadamu amekikosa na anakitafuta mno .....

Kuna kitu anakitafuta ambacho anazani kimebeba furaha yake timilifu, hivyo amejaribu kuitafuta kwa namna mbalimbali lakini namna zote alizotumia zimekuwa hazizai matokeo chanya. Amejaribu kuitafuta furaha kwenye starehe mbalimbali lakini bado ameishia kucheka mdomoni na kubaki na huzuni moyoni.

Utakubaliana na mimi kuwa huwezi kukifahamu kifaa vizuri kama hujasoma maelezo ya aliye kitengeneza, kama kifaa hakifanyi kazi vizuri ni muhimu kurudi na kusoma kifaa kilitengenezwaje na kilibuniwa kifanyeje kazi katika mazingira gani?

Aliyemtengeneza mwanadamu ni Mungu, mwanadamu anapokosa vitu fulani muhimu huwa anaona hakuna uthamani katika kuishi na hili ni tatizo je tunalitatuaje? Ni muhimu turudi kwenye maelekezo ya muumbaji na tuone mwanadamu alibuniwa kuishi kwa namna gani na kwa mazingira gani na anahitaj nini sasa ili aone thamani ya kuishi.

Mathayo 13:45-46,

Tena ufalme wa mbinguni umefanana na mfanya biashara , mwenye kutafuta lulu nzuri; 46 naye alipoona lulu moja ya thamani kubwa, alikwenda akauza alivyo navyo vyote , akainunua.

Kitu cha thamani na muhimu mwanadamu alichokipoteza ni mamlaka au nguvu ya kutawala,nguvu ya kutawala inasababishwa pale mwanadamu anapokuwa ameunganika na Mungu.

Ufalme ni mamlaka, nguvu, uwezo au serikali . Habari njema ya Yesu Kristo ilikuwa ni juu ya ufalme, kwasababu ndicho kitu pekee na muhimu mwanadamu alichokipoteza pale bustani ya Edeni na ndicho kitu wanadamu wanakitafuta hata leo.

Thamani ya ufalme wa Mungu kwa mwanadamu ni zaidi ya kila kitu mwanadamu alichowahi kuwa nacho, ni hazina ya kipekee mno ambayo imebeba majibu ya kila kitu ndani yake. Ndiyo maana Kristo akasema ukitafuta ufalme wa Mungu na haki yake yote huna haja ya kuangaika na vitu vingine vya mwilini kwa sababu ufalme umevibeba ndani yake.

Mathayo 13:44

Tena ufalme wa mbinguni umefanana na hazina katika shamba; ambayo mtu alipoiona, akaificha; na kwa furaha yake akauza alivyonavyo vyote akalinunua shamba lile.

Mahitaji yetu yote tunayohangaika nayo leo yanaweza kutimizwa endapo tukipata hazina hii.

Mathayo 6:33

Bali utafuteni kwanza ufalme wake , na haki yake ; na hayo yote mtazidishiwa.

Yesu anasema “utafuteni” akimaanisha kwamba hatuwezi kuwa na ufalme wa Mungu kama hatuna juhudi ya kutafuta. Kwamba ni vigumu kuingia

sehemu fulani na ukaijua kwa gafra, ni lazima uichunguze , uishi hapo, uone watu wa hapo wanafanya nini, hiyo yote ni kutafuata il ujue kwa uzuri sehemu hiyo.

Kwa kadri tunavyo mtafuta Mungu ndivyo tunavyozidi kumfahamu na kujazwa na nguvu zake na ndivyo ufame wake unavyoweka mizizi imara ndani yetu.

Ukipata ufalme umepata mahitaji yako yote, umepata majibu ya maswali yako yote, umepata utatuzi wa matatizo yako yote.

Furaha yako timilifu imo ndani ya Mungu, ukimtafuta Mungu utaipata furaha yako, ukihitaji furaha usiitafute kokote kule isipokuwa ndani ya Mungu.

Mungu alijua kuwa chanzo cha matatizo ya mwanadamu ni kukaa mbali naye hivyo ili ayatatue hayo matatizo ilikuwa ni lazima alejeshe uhusiano wake na wanadamu ili mwanadamu afanikiwe tena. Hii ndiyo kazi haswa mwana wa Mungu alikuja kuifanya ulimwenguni.

Uhitaji wa asili wa mwanadamu ni Mungu. Ndani ya Mungu ndipo mwanadamu anaweza kuiona thamani yake, furaha yake, utimilifu wa mahitaji yake, kujitambua yeye ni nani, kujua kusudi la uwepo wake, kujua wajibu wake na kuifahamu hatima yake.

Mwanadamu anapokuwa mbali na Mungu huvipoteza hivyo vyote na kusababisha maafa makubwa duniani, mwanadamu anaishi lakini haoni maana ya kuishi. Mungu pekee ndiye anayeweza kukuonyesha thamani ya maisha kwasababu yeye ndiye aliyekuumba na alikuumba kwa kusudi maalum.

UHITAJI WA MWANADAMU HASWA.

Mwanadamu anatafuta haswa kitu kinachoitwa mamlaka (inayotokana na uwepo wa Mungu) ambayo aliipoteza pale alipotengana na Mungu.

Uhitaji wa mwanadamu si dini! Ingawa kwa muda mrefu watu wamekuwa wakiitumia dini ili wakidhi mahitaji yao ya ndani haswa kumkaribia Mungu lakini bado wameishia kukaa mbali na Mungu. Mfano mzuri ni Mafarisayo na viongozi mbalimbali wa dini kipindi cha Yesu, walidai wanamjua Mungu na huku kanashindwa kumtambua Yesu ni nani.

Dini ni juhudi za mwanadamu kumkaribia au kumtafuta Mungu, Baba yangu wa kiroho alinifundisha kuwa wakati mwingine sio juhudi za kumtafuta Mungu kwa wengine wametumia dini kutafuta wanavyovitafuta na si Mungu.

Na kipindi kirefu mwanadamu amekuwa akihangaika na dini mpaka Masihi alipokuja ulimwenguni,Yesu alpozaliwa alizikuta dini. Lakini Mungu ni wa huruma na upendo akaona jinsi mwanadamu anavyoteswa na dini, ndipo akatuletea mfumo mpya ambao sasa sio mwanadamu anayemtafuta Mungu kwanza bali Mungu ndiye anayemtafuta mwanadamu kwanza, hii ndiyo habari njema ya ufalme wa Mungu.

Kama dini ni juhudi za mwanadamu kumtafuta Mungu basi habari njema ya ufalme wa Mungu ni juhudi za Mungu kumtafuta mwanadamu. Huu ndio mfumo uliyofaulu zaidi ya mifumo yote iliyowahi kuanzishwa ulimwenguni.

Mungu aliamua kutufikia kupitia mwanaye Yesu kristo, na yeye ndiye mwongozo pekee wa kumfikia Mungu, anasema katika Yohana 14:6 “mimi ndimi njia, na kweli ,na uzima; Mtu haji kwa Baba, ila kwa njia ya mimi.”

Kupitia Kristo Yesu ndipo tunaona juhudi za kipekee kuhusu Mungu kumtafuta mwanadamu. Anasema “Tazama nasimama mlangoni nagonga

mtu akiisikia sauti yangu na kunifungulia nitaingia kwake na nitakula pamoja nayeye pamoja nami". Ufunuo wa yohana 3:20.

Yesu anasema nalikuja kutafuta kilicho potea, hapa anathibitisha wazi kuwa alikuja kumtafuta mwanadamu aliyekwenda mbali na uwepo wa Mungu, na huu ndio wokovu wa kweli kwasababu hakuna mtu anayemjua mwanadamu na mahitaji yake zaidi ya Mungu aliyemuumba. Tunapata uhakika wa juhudi za Mungu kumtafuta mwanadamu kwasababu anakitu cha muhimu ambacho mwanadamu anakihitaji na mwanadamu akikipata hicho haja yake na kiu yake itapona.

Yeye ndio maji ya uzima ambayo mwanadamu amekuwa na kiu nayo siku zote, anaalika kuwa njooni munywe ili musiwe na kiu tena. Anasema yeye ndiyo chakula cha uzima ambacho mtu akila hata pata njaa tena. Haya yote anayasema kuonyesha kuwa yeye ndiye kitu pekee ambacho mwanadamu alikuwa anakitafuta siku zote na kupitia yeye mwanadamu atakipata kitu hicho.

Hivyo kupitia Yesu Kristo tunarejeshewa mamlaka ya kutawala dunia tena, tunarejeshewa uwepo wa Mungu ndani ya maisha yetu tena. Sasa tunaweza kupambana na kila kitu kilichokuwa kinatutesa kwanza kama vile laana, magonjwa, mapepo, na kila aina ya matatizo yaliyotusumbua hapo awali. Vilivyokuwa vimeshindikana kwanza sasa vinawezekana kupitia Kristo Yesu, vilivyokuwa vigumu mwanzo sasa ni vyepesi, sasa mwanadamu anaweza kutawala tena duniani.

Hivyo uhitaji haswa wa mwanadamu sio kuwa na dini ila kupata mamlaka tena ya kifalme yaani kutawala na kumiliki. Na Kristo alikuja kumrejeshea mwanadamu hicho.

Haja ya kila mtu ni kushinda vikwazo vinavyomsumbua kama magonjwa, hali za uchumi, upweke, manyanyaso, matatizo ya ndoa n.k. Habari njema ni

kuwa huwezi kupata suruhisho la hayo matatizo kupitia dini bali kwa kupitia njia pekee aliyoitengeneza Mungu mwenyewe yaani kupitia Yesu.

Kupitia Kristo utapata haja ya moyo wako na utajazwa na furaha tele. Dini haimpi mtu furaha ila naweza kusema kuwa huwenda ikachangia kwa sehemu kubwa kuondoa furaha ya wengi lakini ufalme wa Mungu upo ili ikutimizie furaha yako tena kwa utimilifu wote.

Yesu anasema nira yangu ni laini na mzigo wangu ni mwepesi (mathayo 11:30 ) hapa alimaanisha kuwa mzigo wake ni mwepesi kwasababu ndio mzigo au kitu pekee ambacho Mungu alikitengeneza ili mwanadamu akibebe nahicho ni uwepo wa Mungu nje ya kitu hicho ni mateso kwa mwanadamu kwasababu Mungu akumtengenezea mwanadamu abebe kitu kingine zaidi ya hicho, ndio maana tunasema dhambi ni mzigo mzito kwasababu Mungu hakumtengenezea mwanadamu ili aubebe. Mungu alimtengeneza mwanadamu ili abebe uwepo na utukufu wake nje ya hapo ni uharibifu kwa mwanadamu.

## KAA TAYARI

Kama Mungu mwenyewe ameamua kutuletea habari njema za ufalme wake yeye mwenyewe sisi tunachopaswa na wajibu wetu ni kuupokea ufalme na kuuishi ufalme.

Kwakuwa tulikuwa tumetoka kwenye mpango wa Mungu aliyokuwa ametuwekea kwanza tunapaswa kurejea kwenye mpango wake, ili kurejea inahitajika jitihada ya ziada ili tukae katika mpango kamili wa Mungu.

Mathayo 11:12

Tangu siku za Yohana Mbatizaji hata sasa ufalme wa mbinguni hupatikana kwa nguvu, nao wenye nguvu wauteka.

Ndiyo Kristo katuletea wokovu lakini yahitajika bidii ili kufaidi matunda ya huo wokovu, unakuhitaji uamue na ujiandae ili upokee utendaji wa Mungu mwenyewe kwenye maisha yako.

Kaa tayari kupokea majibu ya matatizo yako, kaa tayari kupokea nguvu mpya, kaa tayari kupokea uweza wa tofauti, kaa tayari kuhudumwa na Mungu mwenyewe.

Inapoteka maana yake kile ulichokiteka kinafanya kazi kwa ajili yako, unapouteka ufalme maana yake ufalme unafanya kazi kwa ajili yako. Hivyo tegemea utendaji kazi wa tofauti na vile ulivyowahi kuona  mwanzo.

Wanafunzi walipokuwa wakishangaa miujiza aliyokuwa akiifanya Yesu, Yesu aliwatoa wasiwasi na kuwaambia kuwa wao watafanya miujiza mikubwa kuliko ile walioiona Yesu akiifanya. Ni kweli tunaona katika kitabu cha matendo ya mitume matendo makuu ambayo waliyafanya wakina Petro kupitia nguvu za Roho Mtakatifu, kuna wakati waliponya wagonjwa kwa vivuli vyao tu. Matendo ya mitume 5:15

Sasa si wakati wa kuitumikia dini tena ila kuutafuta uso wa Mungu ili ajifunue kwetu, ni hasara kuitumikia dini, kwa kuwa hakuna mahali katika neno la Mungu kuna ahadi juu ya wale wanaozitumikia vizuri dini zao, ila kuna ahadi bora juu ya wale walioukubali ufalme wa Mungu na kuuishi. Heri yao wale watakao jenga nyumba zao kwenye mwamba kwasababu hawata pata hasara kamwe.

Heri yao wale wenye Mungu ndani yao na wala si dini kwa sababu watakuwa wamekaa kwenye kusudi kamili la Mungu, Yesu hakuleta dini ulimwenguni ila ufalme wa Mungu, kwasababu aliona dini haina uwezo wa kumuokoa mwanadamu juu ya mateso yanayomsumbua.

Paulo alikuwa ni mtu wa dini (Paulo alikuwa ni falisayo) lakini dini yake haikumsaidia hadi alipoupokea ufalme wa Mungu ndani yake, pamoja na

kuwa na dini lakini alikuwa ni mtu wa chuki, mwuaji, mwongo na mambo mengi ya machukizo aliyafanya, lakini siku alipompokea mfalme ndani yake maisha yake yakabadilika, Paulo akawa ni mtu mwenye huruma, anayejali wengine na kuwahudumia n.k.

1 timotheo 1:13

Kinachoweza kumbadilisha mtu sio dini ila ni kitu kingine chenye utamaduni tofauti na dini, ufalme wa Mungu ni utawala wenye utamaduni wa tofauti kabisa, ukiingia ndani ya mtu humbadilisha na kumfanya kuwa mtu bora zaidi. Utofauti wa sauli na Paulo ni mabadiliko kutoka kwenye udini kuja kuwa mwana wa ufalme.

Mifumo ya wanadamu bado haina majibu, basi tupate wapi majibu ? basi na tunyanyue macho yetu tutazame kule kwa yeye mwenye majibu. Kaa tayari kuupokea ufalme wa Mungu.

Unajua kwanini watu walimfuata na kumpenda Yesu? Kwasababu yeye ndiye Adamu wa pili, Yesu ndiye mwanadamu pekee aliyeonyesha uhalisia wa vile Adamu wa kwanza alikuwa kabla ya anguko.

Yesu aliweza kutiisha vitu na vikamtii, alionyesha mamlaka juu ya dunia, kwamba anaweza kufanya chochote duniani kwa sababu Mungu kampa mamlaka ya kutawala. Habari njema ni kuwa alijitoa sadaka ili akurejeshee mamlaka hiyo, kaa tayari kuipokea mamlaka, ni kwa ajili yako.

Utaweza kuyadhibiti matatizo yako tena, utaweza kutawala tena, utaweza kufanikiwa tena kwasababu Yesu alikuja kwa ajili hii.